Usulibisho
(The Crucifixion)

Na

Ellis P. Forsman

Usulibisho

Na

Ellis P. Forsman

Oktoba 15, 2011

Usulubisho

Luka 23:1-25

Luka 23:1-25,"*Wakasimama mkutano wote, wakampeleka kwa Pilato. Wakaanza kumshitaki wakisema tumemwona huyu akipotosha taifa letu, na kuwazuia watu wasimpe Kaisari kodi, akisema kwamba yeye mwenyewe ni Kristo mfalme. Pilato akamwuliza akisema wewe ndiwe mfalme wa Wayahudi? Akajibu akamwambia wewe wasema. Pilato akawaambia wakuu wa Makuhani na makutano sioni neno lililo ovu katika mtu huyu. Nao walikaza sana wakisema huwataharakisha watu, akifundisha katika Uyahudi yote, tokea Galilaya mpaka huku. Pilato aliposikia hayo aliuliza kama huyu ni mtu wa Galilaya. Na alipopata habari ya kuwa yu chini ya mamlaka ya Herode, alimpeleka kwa Herode, kwa kuwa yeye naye alikuwako Yerusalemu siku zile. Na Herode alipomwona Yesu alifurahi sana, kwa maana alikuwa akitaka sana kumwona tangu siku nyingi maana amesikia habari zake, akataraji kuona ishara iliyofanywa na yeye. Akamwuliza maneno mengi sana yeye asimjibu lo lote. Wakuu wa Makuhani na waandishi wakasimama wakamshitaki kwa nguvu sana. Basi Herode akamfanya duni pamoja na askari zake, akamdhihaki na kumvika mavazi mazuri; kasha akamrudisha kwa Pilato. Basi siku ile ile Herode na Pilato walipatana kwa urafiki kwa maana hapo kwanza walikuwa na uadui wao kwa wao. Na Pilato akawakutanisha wakuu wa makuhani, na wakubwa na watu akawaambia mtu huyu mmemleta kwangu kana kwamba anapotosha watu; nami tazama nimeamua mambo yake mbele yenu, ila sikuona kwake kosa lo lote katika mambo hayo mliyomshitaki; wala hata Herode kwa maana amemrudisha kwetu basi tazama hakuna nene lo lote alilolitenda lipasalo kufa. Kwa hiyo nitamrudi kasha nitamfungua. [Maana ilimlazimu kuwafungulia mfungwa mmoja wakati wa sikukuu.] Wakapiga kelele wote pamoja, wakisema mwondoe huyu, utufungulie Baraba. Naye ni mtu aliyetupwa gerezani kwa ajili ya fitina iliyotokea mjini na uuaji. Basi Pilato alisema nao mara ya pili, kwa vile alivyotaka kumfungua Yesu. Lakini wakapiga kelele wakisema msulibishe. Msulibishe. Akawaambia mara ya tatu, kwa sababu gani? Huyu ametenda uovu gani? Sikuona kwake hata neno lipasalo kufa. Basi nikiisha kumrudi nitamfungua. Lakini wakatoa sauti zao kwa nguvu sana, wakitaka asulibiwe. Sauti zao zikashinda. Pilato akahukumu kwamba haja yao ifanyike. Akamfungua Yule aliyetupwa gerezani kwa ajili ya fitina na uuaji, Yule waliyemtaka, akamtoa Yesu wamfanyie watakavyo.*"

Yesu anawaambia wanafunzi wake kujiandaa kwa ajili ya Pasaka

Marko 14:12-16, "*Hata siku ya kwanza ya mikate isiyochachwa, walipoichinja pasaka wanafunzi wake wakamwambia, ni wapi utakapo tuende tukuandalie uile pasaka? Akatuma wawili katika wanafunzi wake, akawaambia nendeni zenu mjini; atakutana nanyi mwanamume amechukua mtungi wa maji mfuateni; nap o pote atakapoingia, mwambieni mwenye nyumba, Mwalimu asema ki wapi chumba change cha wageni niile pasaka humo pamoja na wanafunzi wangu? Naye mwenyewe atawaonyesha orofa kubwa, imeandikwa tayari; humio tuandalieni. Wanafunzi wakatoka wakaenda mjini, wakaona kama alivyowaambia, wakaiandaa pasaka.*"

Kihistoria, wayahudi waliandaa pasaka wakati wa masaa ya Kiyahudi saa 9 hadi 12; huo ni, muda uliowekwa na Wayahudi wakati wa Kristo. Nyakati za zamani walikuwa na wakati tofauti za kutunzia muda. Maandalio ya Pasaka kwa nyakati za siku hizi ni kati ya mchana hadi 12 jioni.

Vipi Kuhusu Pasaka?

Ni neno la Kibiblia?

Sawa, ndiyo au hapana. Inaonekana katika Biblia ya KJV.

Mdo. 12:4, "*Alipokwisha kumkamata akamweka gerezani akamtia mikononi mwa vikosi vinne vya askari wanne wanne wamlinde, akitaka baada ya Pasaka kumtoa na kumweka mbele ya watu.*"

3957 pascha {pas' – khah} katika KJV imetafsiriwa kama "Pasaka" mara 28 na "Pasaka" mara 1.

Pasaka ilikuwa ni siku ambayo Wayahudi walisheherekea kupita juu kwa malaika wa kifo walipokuwa utumwani Misri wakati wa Musa.

Pasaka na Uanzilishi wa Meza Ya Bwana

Mat. 26:20-30, "*Basi palipokuwa jioni aliketi chakulani pamoja na wale Thenashara. Nao walipokuwa wakila alisema amin nawaambia mmoja wenu atanisaliti. Wakahuzunika sana wakaanza kumwuliza mmoja mmoja, ni mimi Bwana? Akajibu akasema yeye aliyetia mkono wake pamoja nami katika kombe, ndiye*

atakayenisaliti. Mwana wa Adamu aenda zake, kama alivyoandikiwa lakini ole wake mtu Yule ambaye amsaliti Mwana wa Adamu! Ingekuwa heri kwake mtu yule kama asingalizaliwa. Yuda, yule mwenye kumsaliti akajibu akasema, ni mimi Rabi? Akamwambia wewe umesema. Nao walipokuwa wakila Yesu alitwaa mkate akabariki, akaumega, akawaambia wanafunzi wake, akasema, twaeni mle huu ndio mwili wangu, akakitwaa kikombe akashukuru akisema nyweni nyote katika hiki; kwa maana hii ndiyo damu yangu ya agano imwagikayo kwa ajili ya wengi kwa ondoleo la dhambi. Lakini nawaambieni, sitakunywa kabisa tangu sasa uzao huu wa mzabibu hata siku ile nitakapokunywa mpya pamoja nanyi katika ufalme wa Baba yangu. Nao walipokwisha kuimba wakatoka nje kwenda mlima wa Mizeituni."

Bustani ya Gethsemane.

- Marko 14:26, "*Nao walipokwisha kuimba wakatoka nje kwenda mlima wa Mizeituni.*"
- Marko 14:32-37, "*Kisha wakaja mpaka bustani iitwayo Gethsemane; akawaambia wanafunzi wake, ketini hapa muda niombapo. Akamtwaa Petro na Yakobo na Yohana pamoja naye, akaanza kufadhaika sana na kuhangaika. Akawaambia Roho yangu ina huzuni nyingi kiasi cha kufa; kaeni hapa mkeshe. Akaendelea mbele kidogo akaanguka kifudifudi, akiomba ya kuwa ikiwezekana saa hiyo imwepuke. Akasema Aba, Babayote yawezekana kwako; uniondolee kikombe hiki walakini si kama nitakavyo mimi, bali utakavyo wewe. Akaja akawakuta wamelala usingizi, akamwaambia Petro, Je! Simoni, umelala? Hukuweza kukesha saa moja?*"
- Luka anaongezea: Luka 22:44, "*Naye kwa vile alivyokuwa katika dhiki, akazidi sana kuomba hari yake ikawa kama matone ya damu yakidondoka chini.*"

Dk. Truman Davis anaeleza kwamba takwimu za kitabibu zinaonyesha kwamba hata kama ni chache, hii imetokea pale ambapo mtu yuko katika mshituko mkuu wa hisia. Mishipa midogomidogo iliyoko katika mfumo unaosababisha jasho zinaweza kupasuka, ikisababisha jasho na damu kuchanganyikana. Katika shauri nyingi (sio yote) wakati hili linapotokea, mtu anakuwa na udhaifu na mshituko.

Yesu alijua kuwa alikuwa anakaribia kukabiliwa na usulibisho. Hii ilitokea wakati Fulani usiku wa saa sita.

Marko 14:38-42, "*Kesheni mwombe msije mkaingia majaribuni, roho I radhi ila mwili ni dhaifu. Akaenda zake tena akaomba akisema*

neno lilo hilo. Akaja tena akawakuta wamelala, maana macho yao yamekuwa mazito, wala hawakujua la kumjibu. Akaja mara ya tatu akawaambia laleni sasa mpumzike; yatosha, saa imekuja tazama Mwana wa Adamu anatiwa mikononi mwa wenye dhambi. Ondokeni twendeni zetu; tazama yule anayenisaliti amekaribia."

- Marko 14:43-45, "*Basi alipokuwa katika kusema mara Yuda alifika, mmoja wa wale Thenashara na pamoja naye mkutano, wana panga na marungu, wametoka kwa wakuu wa makuhani na waandishi na wazee. Na yule anayemsaliti alikuwa amewapa ishara, akisema nitakaye mbusu huyo ndiye; mkamateni mkamchukue salama. Basi alipokuja mara akamwendea akasema, Rabi, akambusu.*"
- Luka anaongeza, Luka 22:48, "*Yesu akamwambia, Yuda wamsaliti Mwana wa Adamu kwa kumbusu?*"
- Yoh. 18:3-12, "*Basi Yuda akiisha kupokea kikosi cha askari na watumishi waliotoka kwa wakuu wa makuhani na Mafarisayo akaenda huko na taa na mienge na silaha. Basi Yesu hali akijua yote yatakayompata, akatokea akawaambia ni nani manayemtafuta? Wao wakamjibu ni Yesu Mnazareti. Yesu akawaambia ni mimi. Yuda naye aliyemsaliti alikuwa amesiamama pamoja nao. Basi alipowaambia, ni mimi, walirudi nyuma wakaanguka chini. Basi akawauliza tena, mnamtafuta nani? Wakasema Yesu Mnazareti. Yesu akajibu, nimekwisha kuwaambieni ya kwamba ni mimi, ; basi ikiwa mnanitafuta mimi, waacheni hawa waende zao. Ili litimizwe lile neno alilolisema, wale ul ionipa sikumpoteza hata mmoja wao. Basi Simoni Petro alikuwa na upanga, akaufuta akampiga mtumwa wa kuhani mkuu, akamkata sikio la kuume. Na yule mtumwa jina lake ni Malko. Basi Yesu akamwambia Petro, rudisha upanga alani mwake; je, kikombe alichonipa Baba mimi nisikinywee? Basi wale askari na yule jemadari na wale watumishi wa Wayahudi walimkamata Yesu, wakamfunga.*"
- Mathayo anaongeza, Mat.26:52, "*Ndipo Yesu akamwambia rudisha upanga wako mahali pake, maana wote waushikao upanga wataangamia kwa upanga.*"

Yesu Alipelekwa Mbele Ya Anasi

Usiku uliofuata Petro, alisimama kwa mbali ndani ya hekalu akitazama.

Alikataa kwamba hakumjua Yesu mara tatu, alafu jogoo akawika. Akatoka nje na akalia kwa uchungu.

- Marko 14:55-60, "*Basi wakuu wa Makuhani na baraza yote wakatafuta ushuhuda juu ya Yesu wapate kumwua; wasione. Kwa maana wengi walimshuhudia uongo, walakini ushuhuda wao haukupatana. Hata wengine wakasimama wakamshuhudia uongo wakisema, sisi tulimsikia akisema mimi nitalivunja hekalu hili lililofanyika kwa mikono, na katika siku tatu nitajenga jingine lisilofanyika kwa mikono. Wala hata hivi ushuhuda wao haukupatana. Kasha Kuhani Mkuu akasimama katikati, akamwuliza Yesu akisema hujibu neno? Hawa wanakushuhudia nini?*"

- Yoh. 18:20-24, "*Yesu akamjibu, mimi nimesema na ulimwengu waziwazi; siku zote nalifundisha katika sinagogi na katika hekalu wakusanyikapo Wayahudi wote; wala kwa siri mimi sikusema neno lo lote. Ya nini kuniuliza mimi? Waulize wale walio sikia ni nini niliyowaambia; wao wanajua niliyoyanena. Basi ali[posema hayo mtumishi mmoja wapo aliyesimama karibu alimpiga Yesu kofi akisema wamjibu huvi Kuhani Mkuu. Yesu akamjibu, kama nimesema vibaya ushuhudie ule ubaya; bali kama nimesema vyema wanipigia nini? Basi Anasi akampeleka hali amefungwa kwa Kayafa Kuhani Mkuu.*"

Yesu Mbele Ya Kuhani Alafu kwa Wazee wa Baraza

- Mat. 26:63-68, "*Lakini Yesu akanyamaza. Kuhani Mkuu akamwambia nakuapisha kwa Mungu aliye hai utuambie kama wewe ndiwe Kristo, Mwana wa Mungu. Yesu akamwambia wewe umesema; lakini nawaambieni tangu sasa mtamwona Mwana wa Adamu ameketi mkono wa kuume wa nguvu, akija juu ya mawingu ya mbinguni. Ndipo Kuhani Mkuu akararua mavazi yake akisema, amekufuru mna haja gani tena ya mashahidi? Tazameni sasa mmesikia hiyo kufuru yake; mwaonaje ninyi? Wakajibu wakasema imempasa kuuawa.* (Luka 22:64 inasema Wakamfunika macho)*Ndipo wakamtemea mate ya uso, wakampiga makonde wengine wakampiga makofi, wakisema ewe Kristo tufumbulie ni nani aliyekupiga?*"

- Luka 22:65-71, "*Wakamtolea na maneno mengine mengi ya kumtukana. Hata kulipokucha walikutanika jamii ya wazee,*

na wakuu wa makuhani na waandishi wakamleta katika baraza yao wakisema, kama wewe ndiwe Kristo tuambie. Akawaambia nijapowaambia hamtasadiki kabisa. Tena nikiwauliza hamtajibu. Lakini tangu sasa Mwana wa Adamu atakuwa ameketi upande wa kuume wa Mungu Mwenyezi. Wakasema wote, basi wewe ndiwe Mwana wa Mungu? Akawaambia, ninyi mwasema kwamba mimi ndiye. Wakasema basi tuna haja gani tena ya ushuhuda? Maana sisi wenyewe tumesikia maneno ya kinywa chake?"

Yesu Anapelekwa Mbele Ya Pilato

- Yohana 18:28-38, "*Kisha wakamchukua Yesu kutoka kwa Kayafa mpaka Praitorio, nayo ikawa alfajiri, lakini wao wenyewe hawakuingia ndani ya ile Praitorio, wasije wakanajisika, bali wapate kuila Pasaka. Basi Pilato akawatokea nje akasema, ni mashitaka gani mnayoleta juu ya mtu huyu? Wakajibu wakamwambia, kama huyu asingekuwa mtenda mabaya tusingemleta kwako. Basi Pilato akawaambia haya mtwaeni ninyi mkamhukumu kwa ile torati yenu! Wayahudi wakamwambia sisi hatuna ruhusa ya kuua mtu.* (Josephus – na Agano la Kale wote wanasema kwamba Wayahudi walifanya usulubisho, lakini ilikemewa na kiongozi wa Wayahudi Jannaeus katika mwaka wa 76 BC., hata kama imeandikwa kwamba Wayahudi kweli walifanya usulibisho katika karne ya 2 BC. Usulubisho wa Yesu uliendeshwa na Warumi kwa msisitizo wa Wayahudi.)*Ili litimie lile neno lake Yesu alilolisema, akionyesha ni mauti gani atakayokufa. Basi Pilato akaingia tena ndani ta Praitorio, akamwita Yesu akamwambia, je! Wewe ni Mfalme wa Wayahudi? Yesu akamjibu, wewe wasema hivi kwa nafsi yako, au watu wengine walikwambia habari zangu? Pilato akajibu, Ama! Ni Myahudi mimi! Taifa lako na wakuu wa makuhani ndio waliokuleta kwangu. Umefanya nini? Yesu akajibu ufalme wangu sio wa ulimwengu huu. Kama ufalme wangu ungekuwa wa ulimwengu huu watumishi wangu wangenipigania, nisije nikatiwa mikononi mwa wayahudi. Lakini ufalme wangu sio wa hapa. Basi Pilato akamwambia wewe u mfalme basi? Yesu akajibu, wewe wasema kwa kuwa mimi ni mfalme. Mimi nimezaliwa kwa ajili ya haya, na kwa ajili ya haya mimi nalikuja ulimwenguni, ili niishuhudie kweli. Kila aliye wa hiyo kweli hunisikia sauti yangu. Pilato akamwambia kweli ni nini? Naye akiisha kusema neno hilo*

akawatokea Wayahudi tena, akawaambia mimi sioni hatia yo yote kwake."

- Unaweza kusoma kifungu chote cha Luka kuhusiana na Yesu kushitakiwa mbele ya Herode (Luka 23:1-25).
- Mat. 27:24-25, "*Basi Pilato alipoona ya kuwa hafai lo lote bali ghasia inazidi tu akatwaa maji akanawa mikono yake mbele ya mkutano, akasema mimi sina hatia katika damu ya mtu huyu mwenye haki; yaangalieni haya ninyi wenyewe. Watu wote wakajibu wakasema damu yake na iwe juu yetu, na juu ya watoto wetu.*"
- Mat. 27:26-30, "*Ndipo akawafungulia Baraba na baada ya kumpiga Yesu mijeledi, akamtoa ili asulibiwe. Ndipo askari wa liwali wakamchukua Yesu ndani ya Praitorio,* [Marko 15:16] inasema sehemu hiyo iliitwa Praitorio) *wakamkusanyikia kikosi kizima. Wakamvua nguo wakamvika vazi jekundu. Wakasokota taji ya miiba wakaiweka juu ya kichwa chake, na mwanzi katika mkono wake wa kuume, wakapiga magoti mbele yake wakamdhihaki, wakisema, Salamu Mfalme wa Wayahudi. Kasha wakamtemea mate, wakautwaa ule mwanzi wakampiga piga kichwani.*"

Upigaji.

Maandalizi ya upigaji yalifanywa wakati mfungwa anachaniwa nguo na mikono yake kufungwa kwenye mti juu ya kichwa chake. Mkuu wa Kirumi anakwenda mbele akiwa na *mwanzi* mkononi mwake. Huu ni mjeledi mfupi ulio na ngozi nyingi nyingi nzito na mifuniko miwili au mifupa iliyofungwa mwishoni mwa kila jeledi. Kiboko hiki kizito huletwa chini kwa nguvu tena na tena ikizunguka mabegani mwa mfungwa, mgongoni na miguuni. Mwanzoni mifuniko hii huchana ngozi pekee. Alafu mapigo yanapoendelea, yanazidi kukata hadi katika mishipa ya fahamu na misuli, ikisababisha ububujikaji wa damu, alafu uvujaji mwingi wa damu. Inapogundulika na mkuu aliyeko madarakani kwamba mfungwa anakaribia kufa, upigaji unashitishwa. Wayahudi walikuwa na sheria kwamba hakuna mtu ambaye angepigwa mara 40 hivyo mara zote walikomea ufupi ili kuhakikisha kwamba hawazidi kiwango hicho. Kulingana na encyclopedia, Warumi ahawakuwa na mfumo huo wa 40 tunza moja.

Taji ya miba.

Hii inatengenezwa kwa mmea ulio maarufu Yerusalemu unaokua futi 4 hadi 8 urefu kwenda juu, ni laini (inaweza

kukunjwa isivunjike), lakini pia inazungukwa na miba midogo-midogo mifupi. Hii iliwekwa juu ya kichwa cha Kristo, alafu ikagongomewa, ikisukuma miba ndani ya fuvu. Fuvu linapotobolewa huvuja sana.

Pilato Anatafuta Kumwachia Yesu

Yohana 19:4-16, "*Kisha Pilato akatokea tena nje, akawaambia mtu huyu namleta nje kwenu, mpate kufahamu ya kuwa mimi sioni hatia yo yote kwake. Ndipo Yesu alipotoka nje naye amevaa ile taji ya miiba na lile vazi la zambarau Pilato akawaambia tazama mtu huyu! Basi wale wakuu wa Makuhani na watumishi wao walipomwona walipiga kelele wakisema Msulibishe! Msulibishe! Pilato akawaambia mtwaeni ninyi basi mkamsulibishe; kwa maana mimi sioni hatia kwake. Wayahudi wakamjibu sisi tunayo sheria, na kwa sheria hiyo amestahili kufa, kwa sababu alijifanya kuwa Mwana wa Mungu. Basi Pilato aliposikia neno hilo akazidi kuogopa. Akaingia tena ndani ya ile Praitorio, akamwambia Yesu wewe umetokapi? Lakini Yesu hakumpa jibu lo lote. Basi Pilato akamwambia husemi nami? Hujui ya kuwa mimi nina mamlaka ya kukufungua, nami nina mamlaka ya kukusulibisha? Yesu akamjibu wewe ungekuwa na mamlaka yo yote juu yangu, kama usingepewa kutoka juu; kwa hiyo yeye aliyenitia mikononi mwako yuna dhambi iliyo kubwa zaidi. Na tangu hapo Pilato akatafuta kumfungua; lakini Wayahudi wakapiga makelele wakisema, ukimfungua huyu wewe si rafiki yake Kaisari; kila mtu ajifanyaye kuwa mfalme humfitini Kaisari, basi Pilato aliposikia maneno hayo akamleta Yesu nje, akaketi juu ya kiti cha hukumu mahali paitwapo Sakafu ya Mawe au kwa Kiebrania Gabatha. Nayo ilikuwa maandalio ya pasaka, yapata saa sita. Akawaambia Wayahudi tazama mfalme wenu! Basi wale wakapiga kelele Mwondoshe! Mwondoshe! Msulibishe! Pilato akawaambia Je! Nimsulibishe mfalme wenu! Wakuu wa makuhani wakamjibu sisi hatuna Mfalme ila Kaisari. Ndipo alipomtia mikononi mwao ili asulibiwe; nao wakampokea Yesu.*"

Njiani Kuelekea Goligotha

Mat. 27:31-34, "*Walipokwisha kumdhihaki, wakalivua lile vazi wakamvika mavavi yake, wakamchukua kumsulibisha. Hata walipokuwa wakitoka wakamwona mtu Mkirene, jina lake Simoni; huyu wakamshurutisha auchukue msalaba wake. Na walipofika mahali paitwapo Golgotha, yaani Fuvu la kichwa, wakampa kunywa divai ilyochanganywa na nyongo, lakini yeye alipoionja hakutaka kunywa.*"

Sehemu ya msalaba ambao Yesu alibeba (kama ilivyo kuwa desturi ya usulibisho) ilikuwa ni ile sehemu ya juu, inayoitwa patibulum. Ilikuwa inafungwa mabegani mwa mfungwa, na alipaswa kuibeba hadi katika sehemu ya usulibisho. Yesu alikuwa dhaifu sana kuweza kuibeba, hivyo Simoni Mkirene alishinikizwa aibebe. Kulingana na Encyclopedia, mti wa msalaba ulio wima, tayari ulikuwa umeshasimikwa ardhini. Mara nyingi nimekuwa nikiwatazama wakiweka msalaba ardhini baada ya kugomewa. Sivyo ilivyo fanywa kulingana na historia.

Kulikuwa na aina nyingi za misalaba iliyotumiwa na Warumi. Aina mbili zilizo maarufu ilikuwa ni muundo uliofanana na T kubwa sehemu ya juu ya msalaba, na nyingine ikiwa na ubao uliokatiza inch chache kutoka juu. Kuna wasomi kutoka kambi zote wanao amini kwamba Kristo alisulibiwa katika mfumo wa kizamani. Sababu inayofanya niamini kwamba ubao wa chini ulitumika (kama ilivyoelezwa na wasomi wengi) ilikuwa kwa sababu ya ishara "MFALME WA WAYAHUDI" iliwekwa kwenye msalaba juu ya kichwa chake.

Hataivyo nyingi ya misalaba iliyotumika iliacha miguu ya watuhumiwa juu kidogo ya ardhi, mirefu pia ilitumika. Wasomi wengi wanaamini kwamba iliyotumika kumsulibisha Yesu ilikuwa futi 7 hadi 9 kwenda juu. Fimbo ya hisopu na sponji iliyojaa siki iliwekwa katika kinywa cha Yesu. Vitabu tofauti husema kuwa fimbo hii ingekuwa na urefu wa futi 3 hadi 4. Fimbo fupi ingekuwa change sana na laini.

- Isa. 52:13, "*Tazama mtumishi wangu atatenda kwa busara, atatukuzwa na kuinuliwa juu naye atakuwa juu sana*"
- Yoh. 3:14, "*Na kama vile Musa alivyomwinua yule nyoka jangwani, vivyo hivyo Mwana wa Adamu hana budi kuinuliwa;*"

Kulikuwa na mifumo nyingi ya kumweka mfungwa kwenye msalaba. Wakati Fulani viganja vyao viligongomewa msalabani huku mikono yao ikiwa imepinda kidogo, wakati Fulani zilifungwa, wakati Fulani zilikuwa zinafungwa na kugongomewa. Misumari ilikuwa inawekwa katika eneo la kiganja katikati ya mifupa miwili ya kiganja. Tunakuta katika Agano la Kale kwamba sehemu hii ya kiganja ilizingatiwa. (Bangili iliwekwa mkononi). Takwimu za kihistoria niliyopata zinasema kwamba wakati Fulani miguu iliachwa ikining'inia, wakati mwingine ilikuwa inafungwa, na wakati mwingine ilikuwa inakazwa kwa misumari iliyogongwa kupitia metatasali (hiyo ni kupitia sehemu ya mfupa wa mguu. (Tarsali alafu mertasali, alafu falanji). Wakati mwingine ubao mdogo unawekwa chini ya miguu ili kumsaidia mtuhumiwa

kujisukuma kwenda juu ili aweze kupumuwa na kuipa mikono yake pumziko. Hii ilifanya maumivu kuwa marefu, kwa mtuhumiwa akiishia siku 3 au zaidi. Yesu alikaa kwa masaa sita tu, hivyo haiaminiki kwamba alikuwa na ubao huo, lakini alilazimika kujisukuma katika misumari iliyo kuwa miguuni pake ili aweze kupumua. Mikono yake ingekuwa na maumivu na kupumua kulikuwa kwa shida kifua kiliuma sana na moyo ukabanwa.

Zaburi 22:14-15, "*Nimemwagika kama maji mifupa yangu yote imeteguka, moyo wangu umekuwa kama nta, na kuyeyuka ndani ya mtima wangu. Nguvu zangu zimekauka kama gae, ulimi wangu waambatana na taya zangu; unaniweka katika mavumbi ya mauti.*"

Kama ukienda Yerusalemu leo, utapata sehemu mbili zinazodaiwa kuwa ndio Golgotha, au sehemu ya fuvu. Sehemu ya kweli ilipaswa kuwa karibu na Yerusalemu, lakini nje ya kuta za mji (sheria ya Kiyahudi), ikionekana tokea mbali (Mat. 27:55 & Marko 15:40), kuwa karibu na barabara (Mat. 27:39, Mk. 15:29), na ina sababu ya kuitwa sehemu ya fuvu. Sehemu ya kwanza (kuitwa Sepchre takatifu) ilidaiwa kuwa sehemu ya Golgotha katika karne ya 4 wakati wa Constantine, wakati Eusebius alipomuagiza Marcarius kutafuta sehemu halisi ya Golgotha. Alidai kufahamu sehemu hiyo ilipokuwa. Kanisa la Constantine liliamuriwa kujegwa katika sehemu hiyo. Leo kanisa la Mtakatifu Sepulchre inakaa katika eneo hilo. Wasomi leo wanasema hiyo haiwezi kuwa sehemu halisi kwa sababu mbili: 1) Haikuwa nje ya kuta ya mji wa zamani, na 2) isingeweza kuonekana tokea mbali. Sehemu ya pili, inayojulikana kama Kalvari ya Gordon, hufanana vyema na maelezo haya yote. Ni sehemu yenye mawe, ikiwa na kila aina ya ukataji tama, wakati Fulani inaweza kufanana na fuvu, na ilitumiwa Wayahudi wa zamani kama sehemu ya kupiga mawe.

Usulibisho

- Mat. 27:35-38, "*Walipokwisha kumsulibisha waligawa mavazi yake, wakipiga kura; [ili litimie neno lililonenwa na nabii waligawa nguo zangu kati yao, na juu ya vazi langu walipiga kura], wakaketi wakamlinda huko. Wakaweka juu ya kichwa chake mashitaka yake yaliyoandikwa HUYU NI YESU, MFALME WA WAYAHUDI. Wakati uo huo wanyang'anyi wawili wakasulibiwa pamoja naye, mmoja mkono wake wa kuume, na mmoja mkono wake wa kushoto.*"
- Yoh. 19:20 inasema kwamba iliandikwa Kiebrania, Kiyunani, na Kilatini.

- Yoh. 19:21-24, "*Basi wakuu wa makuhani na Wayahudi wakamwambia Pilato, usiandike Mfalme wa Wayahudi; bali ya kwamba yule alisema, Mimi ni Mfalme wa Wayahudi. Pilato akajibu niliyoandika nimeyaandika. Nao askari walipomsulibisha Yesu, waliyatwaa mavazi yake wakafanya mafungu manne, kwa kila askari fungu lake; na kanzu nayo. Basi kanzu ile haikushonwa ilikuwa imefumwa yote tangu juu. Basi wakaambiana tusiipasue, lakini tuipigie kura iwe ya nani. Ili litimie andiko lile linenalo, waligawanya nguo zangu, na vazi langu walipigia kura. Basi ndivyo walivyofanya wale askari.*"
- Mat. 27:39-44, "*Nao waliokuwa wakipita njiani wakamtukana wakitikisa tikisa vichwa vyao, wakisema ewe mwenye kulivunja hekalu na kulijenga kwa siku tatu jiokoe nafsi yako ukiwa ndiwe Mwana wa Mungu, shuka msalabani. Kadhalika na wale wakuu wa makuhani wakamdhihaki pamoja na waandishi na wazee wakisema, aliokoa wengine hawezi kujiokoa mwenyewe. Yeye ni mfalme wa Israeli; na ashuke sasa msalabani, nasi tutamwamini. Amemtegemea Mungu na amwokoe sasa, kama anamtaka kwa maana alisema Mimi ni Mwana wa Mungu. Pia wale wanyang'anyi waliosulibiwa pamoja naye walimshutumu vilevile.*"
- Luka 23:40-43, "*Lakini yule wa pili akamjibu akamkemea akisema wewe humwogopi hata Mungu, nawe u katika hukumu iyo hiyo? Nayo ni haki kwetu sisi kwa kuwa tunapokea malipo tuliyostahili kwa matendo yetu; bali huyu hakutenda lo lote lisilofaa. Kasha akasema ee Yesu nikumbuke utakapoingia katika ufalme wako. Yesu akamwambia amini nakuambia leo hivi utakuwa pamoja nami peponi.*"

Paradiso hapa ilikuwa ni Hedis. Haikuwa mbingu. Neno la Kiyunani, "Hedes" (ambayo ni sawa na neno la Kiebrania, "Sheol") ni "kisicho onekana" au sehemu "inayopokea yote" ambapo nafsi za wafu zinapokwenda kusubiri hukumu. Katika Matendo 2:31, Petro ananukuu Zaburi 16:10, "*Maana hutakuachia kuzimu nafsi yangu, wala hutamtoa mtakatifu wako aone uharibifu.*" Kristo hakuenda katika sehemu ya mateso, kwa maana hiyo haijaja bado. Alikwenda katika sehemu ya kusubiria, ambapo Anaita kuwa ni "Paradiso." Baadaye Kristo akasema hajapaa bado kwenda Mbinguni. Akamwambia mwizi alipomwuliza kumkumbuka, "Tutakuwa pamoja wote siku ya leo." Yesu hakumuahidi mwizi wokovu.

Yohana 19:25-27, "*Na penye msalaba wake Yesu walikuwa wamesimama mamaye, na umbu la mamaye, Mariamu wa Klopa, na Mariamu Magdalene. Basi Yesu alipomwona mama yake na yule mwanafunzi aliyempenda amesimama karibu, alimwambia mama yake, mama tazama mwanao. Kasha akamwambia yule mwanafunzi tazama mama yako. Na tangu saa ile mwanafunzi yule akamchukua nyumbani kwake.*"

Kwanzia wakati huo kuendelea Mtume Yohana akaanza kumtunza Mariamu, mama wa Yesu.

- Mat. 27:45-50, "*Basi tangu saa sita palikuwa na giza juu ya nchi yote hata saa tisa. Na kama saa tisa Yesu akapaza sauti yake kwa nguvu akisema, Eloi, Eloi, lama sabakthani? Yaani Mungu wangu Mungu wangu, mbona umeniacha? Na baadhi yao waliohudhuria, waliposikia walisema huyu anamwita Eliya. Mara mmoja wao akaenda mbio akatwaa sifongo, akaijaza siki akaitia juu ya mwanzi, akamnywesha. Wale wengine wakasema, acha na tuone kama Eliya anakuja kumwokoa. Na Yesu akiisha kupaza sauti tena kwa nguvu, akaitoa roho yake.*"

- Yoh. 19:28-30, "*Baada ya hayo Yesu hali akijua ya kuwa yote yamekwisha kumalizika ili andiko litimizwe, akasema naona kiu. Kulikuwako huko chombo kimejaa siki; basi wakatia sifongo ilijaa siki juu ya ufito wa hisopo wakampelekea kinywani. Basi Yesu alipokwisha kuipokea ile siki, alisema imekwisha. Akainama kichwa chini akaisalimu roho yake.*"

Hisopo.

Yesu alipewa kinywaji: divai iliochanganywa na nyongo, ambayo ilikuwa chungu lakini alikataa. Inavutia kuona kwamba hisopu chini ya Sheria ya Kale ilitumika katika kunyunyiza damu ya mnyama aliyetolewa sadaka, hasa damu ya mwana kondoo.

- Ebr. 9:19-20, "*Maana kila amri ilipokwisha kunenwa na Musa kwa hao watu wote, kama ilivyoamuru sheria, aliitwaa damu ya ndama na ya mbuzi pamoja na maji na sufu nyekundu na hisopo akakinyunyizia kitabu chenyewe, na watu wote, akisema hii ni damu ya agano mlioamriwa na Mungu. Na ile hema yote nayo na vyombo vyote vya ibada alivinyunyizia damu vivyo hivyo.*"

- Kut. 12:22, "*Nanyi twaeni tawi la hisopu mkalichovye katika ile damu iliyo bakulini na kukipiga kizingiti cha juu na miimo miwili ya mlango, kwa hiyo damu iliyo katika bakuli tena mtu*

ye yote miongoni mwenu asitoke mlangoni mwa nyumba yake hata asubuhi."

Giza Limetanda

- Mat. 27:45-46, "*Basi tangu saa sita palikuwa na giza juu ya nchi yote hata saa tisa. Na kama saa tisa, Yesu akapaza sauti yake kwa nguvu akisema, Eloi, Eloi, lamasabakthani? Yaani Mungu wangu, Mungu wangu, mbona umeniacha?*"
- Mat. 27:51-56, "*Na tazama pazia la hekalu likapasuka vipande viwili toka juu hata chini; nchi ikatetemeka miamba ikapasuka; makaburi yakafunuka; ikainuka miili mingi ya watakatifu waliolala; nao wakiisha kutoka makaburini mwao, baada ya kufufuka kwake wakauingia mji mtakatifu, wakawatokea wengi. Basi yule akida na hao waliokuwa pamoja naye wakimlinda Yesu walipoliona tetemeko la nchi na mambo yaliyofanyika, wakaogopa sana wakisema hakika huyu alikuwa Mwana wa Mungu. Palikuwa na wanawake wengi sana pale wakitazama kwa mbali, hao ndio waliomfuata Yesu toka Galilaya, na kumtumikia. Miongoni mwao alikuwamo Mariamu Magdalene, na Mariamu mama yao Yakobo na Yusuph, na mama yao wana wa Zebedayo.*"
- Yoh. 19:31-37, "*Basi Wayahudi kwa kuwa ni maandalio miili isikae juu ya misalaba siku ya sabato, (maana sabato ile ilikuwa siku kubwa), walimwomba Pilato miguu yao ivunjwe wakaondolewe. Basi askari wakaenda wakamvunja miguu wa kwanza na wa pili, aliyesulibiwa pamoja naye. Lakini walipomwijia Yesu na kuona ya kuwa amekwisha kufa hawakumvunja miguu; lakini askari mmoja wapo alimchoma ubavu kwa mkuki na mara ikatoka damu na maji. Naye aliyeona ameshuhudia na ushuhuda wake ni kweli, naye anajua ya kuwa anasema kweli ili ninyi nanyi mpate kusadiki. Kwa maana hayo yalitukia ili andiko litimie, hapana mfupa wake utakaovunjwa. Na tena andiko linguine lanena, watamtazama yeye waliyemchoma.*"

Yesu Alitolewa Msalabani na Kuzikwa

Mat. 27:57-66, "*Hata ilipokuwa jioni akafika mtu tajiri wa Arimathaya, jina lake Yusufu, naye mwenyewe alikuwa mwanafunzi wa Yesu. Mtu huyu alimwendea Pilato akamwomba mwili wa Yesu. Ndipo Pilato akaamuru apewe. Yusufu akautwaa mwili akauzonga zonga katika sanda ya kitani safi, akauweka katika kaburi lake*

jipya, alilokuwa amelichonga mwambani, akaviringisha jiwe kubwa mbele ya mlango wa kaburi, akaenda zake. Na pale walikuwapo Mariamu Magdalene, na Mariamu yule wa pili, wameketi kulielekea kaburi. Hata siku ya pili ndiyo iliyo baada ya maandalio, wakuu wa makuhani na Mafarisayo wakamkusanyikia Pilato, wakasema Bwana tumekumbuka kwamba yule mjanja alisema, alipokuwa akali hai, baada ya siku tatu nitafufuka. Basi amuru kwamba kaburi lilindwe salama hata siku ya tatu; wasije wanafunzi wake wakamwiba na kuwaambia watu amefufuka katika wafu na udanganyifu wa mwisho utapita ule wa kwanza. Pilato akawaambia mna askari nendeni mkalilinde kaburi salama kadiri mjuavyo. Wakaenda wakalilinda salama, kwa kulitia lile jiwe muhuri, pamoja na wale askari walinzi."

Ufufuo

Siku ya kwanza ya juma, Jumapili asubuhi.

Mat. 28:1-7, "*Hata sabato ilipokwisha, ikipambazuka siku ya kwanza ya juma, Mariamu Magdalene, na Mariamu yule wa pili, walikwenda kulitazama kaburi. Na tazama palikuwa na tetemeko kubwa la nchi; kwa sababu malaika wa Bwana alishuka kutoka mbinguni, akaja akaliviringisha lile jiwe akalikalia. Na sura yake ilikuwa kama umeme, na mavazi yake meupe kama theluji. Na kwa kumwogopa wale walinzi wakatetemeka, wakawa kama wafu. Malaika akajibu akawaambia wale wanawake, Msiogope ninyi kwa maana najua mnamtafuta yule aliyesulibiwa. Hayupo hapa kwani ameshafufuka kama alivyosema, njooni mpatazame mahali alipolazwa. Nanyi nendeni upesi mkawaambie wanafunzi wake, amefufuka katika wafu. Tazama atawatangulia kwenda Galilaya, ndiko mtakakomwona. Haya nimekwisha waambia.*"

Kulikuwa bado hakuja pambazuka.

Ukweli kuhusu Sabato

Mat. 12:40, "*Kwani kama vile Yona alivyokuwa siku tatu mchana na usiku katika tumbo la nyangumi, hivyo ndivyo Mwana wa Adamu atakavyokuwa siku tatu mchana na usiku katika moyo wan chi.*"

Wengi wanaamini kwamba Yesu alikufa siku ya Ijumaa kabla Sabato ya Sabato; lakini hii haihusiani na kuzikwa kwake siku tatu mchana na usiku kulingana na Mathayo.

Kutoka Ijumaa jioni hadi juma Pili asubuhi sio siku 3 mchana na usiku.

Kuna jibu la kimaantiki katika hili.

Mlolongo uko katika Mathayo anapoonyesha sikukuu ya Pasaka.

- Mat. 26:1-5, "*Ikawa Yesu alipomaliza maneno hayo yote, aliwaambia wanafunzi wake, mnajua ya kuwa baada ya siku mbili itakuwa Pasaka, na Mwana wa Adamu atasalitiwa asulibiwe. Wakati ule wakuu wa makuhani na wazee wa watu, wakakusanyika katika behewa ya Kuhani Mkuu jina lake Kayafa; wakafanya shauri pamoja, ili wamkamate Yesu kwa hila na kumwua. Lakini wakasema isiwe wakati wa sikukuu isije ikatokea ghasia katika watu.*"

- Yoh. 19:12-15, "*Na tangu hapo Pilato akatafuta kumfungua, lakini Wayahudi wakapiga makelele wakisema ukimfungua huyu wewe si rafiki yake Kaisari; kila mtu ajifanyaye kuwa mfalme humfitini Kaisari. Basi Pilato aliposikia maneno hayo, akamleta Yesu nje akaketi juu ya kiti cha hukumu, mahali paitwapo sakafu yam awe, au kwa Kiebrania Gabatha. Nayo ilikuwa maandalio ya Pasaka yapata saa sita. Akawaambia Wayahudi tazama Mfalme wenu. Basi wale wakapiga kelele, Mwondoshe! Mwondoshe! Msulubishe! Pilato akawaambia je nimsulibishe Mfalme wenu! Wakuu wa makuhani wakamjibu, sisi hatuna mfalme ila Kaisari.*"

- Yoh. 19:31, "*Basi Wayahudi kwa kuwa ni maandalio miili isikae juu ya misalaba siku ya sabato, (maana sabato ile ilikuwa siku kubwa), walimwomba Pilato miguu yao ivunjwe, wakaondolewe.*"

Luka anaeleza wakati mwili wa Yesu ulipoandaliwa kwa kuzikwa bado ilikuwa ni katika maandalizi ya Pasaka na akaiita sabato.

Luka 23:53-54, "*Akaushusha akauzinga sanda ya kitani, akauweka katika kaburi lililochongwa mwambani, ambalo hajalazwa mtu ndani yake. Na siku ile ilikuwa siku ya maandalio, na sabato ikaanza kuingia.*"

Kwa vile Sikukuu ya Sabato mara zote ilitokea katika 14 Nisani (kalenda ya Wayahudi), Yesu alikufa msalabani katika siku ya 13 ya Nisani. Neno sabato kwa Wayahudi inamaanisha siku ya mapumziko. Walipaswa kupumzika katika siku ya Sabato pia. Iliitwa siku ya Sabato kuu.

Ulimwengu wa dini kihistoria wanaonyesha Yesu kufa msalabani katika mwaka wa A.D. 33 kwa sababu katika mwaka huo Nisan 13 ilitokea siku ya Ijumaa. Lakini tarehe ya kimaantiki ya usulibisho wake ilikuwa Alhamisi, Aprili 6 katika mwaka wa A.D. 30.

Uthibitisho zaidi ya Sikukuu ya Pasaka kuitwa sabato.

- Mat. 28:1 Katika toleo la Kiyunani inaeleweka kwamba sabato ni wingi, hata ivyo Biblia ya Mfalme Yakobo inaonyesha kwamba ni katika umoja.
- Mat. 28:1, "*Hata sabato ilipokwisha, ikipambazuka siku ya kwanza ya juma, Mariamu Magdalene, na Mariamu yule wa pili, walikwenda kulitazama kaburi.*"

Toleo la Kiyunani tafsiri halisi linasema, "*mwisho wa sabato…*", hivyo ikijumuisha sabato kuu (Sikukuu ya Pasaka na Pasaka halisi (Jumamosi) vyote kuwa huishia katika siku ya kwanza ya juma.

Siku ya Pentekoste ilikuwa ni siku 50 baada ya sabato ya kwanza ikifuatiwa na Sikukuu ya Pasaka. Mara zote ilikuwa ni katika siku ya kwanza ya jumaa

Hitimisho

Yesu alijitoa mwenyewe kwa wengine wakati wa huduma yake na akajitoa msalabani.

- 1 Pet. 2:21, "*Kwa sababu ndiyo mlioitiwa; maana Kristo naye aliteswa kwa ajili yenu, akawaachia kielelezo mfuate nyayo zake.*"
- Isa. 53:4-6, "*Hakika ameyachukua masikitiko yetu, amejitwika huzuni zetu; lakini tulimdhania ya kuwa amepigwa, amepigwa na Mungu na kuteswa. Bali alijeruhiwa kwa makosa yetu, alichubuliwa kwa maovu yetu; adhabu ya amani yetu ilikuwa juu yake, na kwa kupigwa kwake sisi tumepona. Sisi sote kama kondoo tumepotea; kila mmoja wetu amegeukia njia yake mwenyewe; na BWANA ameweka juu yake maovu yetu sisi sote.*"

Tuna mengi ya kushukuru kwa usulibisho aliopitia kwa ajili yetu sote.